



“Leo nyota inayoangaza imeshuka hapa duniani” (Lit. ya Noeli)

*“Tumwabuduu yule aliyeangaza
akili zetu kwa mafundisho yake
na aliyeweka alama ya kusikia kwetu
kwa njia ya maneno yake.
Tumshukuru yeye aliyepandikiza
matunda yake katika mti wetu.
Shukrani kwa yule aliyemtuma mwanaye
mrudhi wake
kutuvuta kwake kwa njia yake
na kutufanya tuwe waridhi pamoja naye.
(S. Efrem il Siro, III Inno sulla natività, IV sec.)*

Ujio wa mkomboizi wetu uangaze kuwepo kwetu ili uangarishwe

kuwa wema na huruma yake.

Pamoja na Masista wote wa Misericordia

Nawatakia heri nyingi ya upendo wa Noeli njema

na mwaka mpyia yenye fanaka na utajiri wa neema na amani.

*madre Maria Visentini
Mama mkuu*

Verona, Noeli 2021

Verona 17.12.2021

Wapendwa ndugu walei wa Misericordia,

nachukua tena sehemu fupi ya utenzi wa Noeli ya S. Efrem, anayetuangaza sababu ya lengo la ujio wa Bwana wetu Yesu Cristo kati yetu.

Ujio wa Yesu, kwa kweli, inatuingiza ndani ya furaha kubwa ya historia ya ukombozi wetu ambao yeye alianza na kukamilisha kwa kila mmoja wetu. Bwana wetu Yesu Cristo alikuja kwa kuangaza safari inayotupeleka kwa Munfgu, katika kupanua akili, fikra na moyo wetu wa kusikiliza Neno lake la ukweli na la uhai; alitujalia nguvu ili Neno lake liwe chemchemi inayochipua matunda ya huruma.

Katika yeye, Mungu alitufanya waridhi wa wema wake na wenye furaha ya maisha ya milele. Fadhili hizi za Bwana ni za wote, kwa sababu tu watoto wake na katika yeye wote tu ndugu kati yetu, kama anavyohibithisha Papa Francasco kwenye barua yake ya kichungaji “Fratelli tutti” au Wote ndugu”.

Katika chemchemi hii tunaitwa kuwa watangazaji wa wema wake, huruma yake kwa maneno na matendo.

Namshukuru Mungu kwa jukumu lenu la kusambaza wema wa Mungu ili watu maskini na wenye shida watambue upendo na wipo wa Mungu kati yao kama walivyofanya wenyeheri wetu baba Carlo na mama Vincenza Maria. Huko Mbinguni awahifadhi, walinde, wawabariki na wawakinge kwa kuwajalia ninyi na familia zenu amani, utulivu ya Noeli hii takatifu na kila wema kwa mwaka 2022.

Pamoja na masista halmashauri wote nawatumia salamu za pekee na za kindugu pamoja na masista wanaosindikiza katika safari yenu.

madre Maria Visentin

Mama mkuu